

UHAKIKI WA VITUO VYA UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA.

Vituo vya kuandikishia wapiga kura ndio msingi wa vituo vya kupigia kura. Uhakiki wa vituo vya kuandikishia wapiga kura hufanyika kabla ya kuanza kwa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga kura.

Kwa kuzingatia kifungu cha 3 cha sharia ya Taifa ya Uchaguzi, sura 343 na kifungu cha 4 cha Sheria ya uchaguzi ya Serikali za Mitaa, sura ya 292 Tume ilitoa mwongozo unaonesha mambo muhimu ya kuzingatiwa wa kati wa utekelezaji wa zoezi la Uhakiki vituo vya kuandikisha wapiga kura.

Halmashauri ya wilaya ya Ngara ilipokea kiasi cha **Tsh 6,760,000.00/=** kwa ajili ya kugharamia zoezi la uhakiki wa Vituo vya Uandikishaji wa wapiga kura mwezi Mei 2018 ikiwa ni maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la wapiga kura katika wilayaya Ngara.

Aidha, **TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI (NEC)** ilituma fedha hizi pamoja na mchanganuo wa matumizi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya matumizi ya Fedha.

Taarifa ya vituo vya kupigia kura kwa kata 22 katika Halmashauri ya wilaya ya Ngara mwaka 2015 jumla ilikuwa vituo 216 na jumla ya idadi ya vituo vya kupigia kura vilivyohakikiwa mwaka 2018 ni 216 kwa ajili ya maandalizi ya Uboreshaji wa Daftari la wapiga kura.